



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA
JIMBO LA KWIMBA NA SUMVE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MZA/KDC/CCL.20/1/VOL.III/165.

TAREHE: 21/09/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la **KWIMBA NA SUMVE** kwa kuzingatia kanuni ya 14 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Watendaji wa Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kama ifuatavyo:-

- 1. Msimamiziwa Kituo cha Kupigia Kura (Nafasi 575).**
 - 2. Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura (Nafasi 1150).**
 - 3. Karani Mwongozaji wapiga Kura (Nafasi 575).**
- A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
 - (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
 - (c) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na

(e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba.

**B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI ZA KARANI
MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**

(a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;

(b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;

(c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanyia kazi

(d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

(e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na

(f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo:-

- i. Msimamizi wa Kituo siku ya Uchaguzi atalipwa posho ya Tzs. **35,000** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs **15,000** kwa siku moja na nauli Tzs **20,000**;
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Tzs. **30,000** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs **15,000** na nauli Tzs **20,000**; na
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Tzs **30,000** kwa siku moja na posho ya chakula Tzs **15,000**.

D. MASHARITI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.

- Maombi yote yaambatane na Vyeti vya taaluma, nakala za Vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa kwa mujibu wa Tangazo hili.
- Waombaji waambatishe picha mbili 'Passport size' za hivi karibuni.
- Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma atapaswa kupitisha maombi kwa mkuu wake wa kazi na Msimamamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Kata. Mwombaji ambae si mtumishi wa Umma, maombi yake yapitie kwa Mtendaji wa Kata na Msimamamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Kata anayoomba kufanya kazi.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Septemba , 2020 saa Tisa na Nusu Alasiri (9:30 Alasiri).**

Waombaji waliowahi kufanya kazi kiustadi katika zoezi la Uchaguzi Mkuu na wanazo sifa zilizotajwa hapo juu watapewa kipaumbele.

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni:-

Msimamamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Kwimba na Sumve
S.L.P 88,

**NGUDU/KWIMBA
Ofisi ya Uchaguzi.**

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA KWIMBA NA SUMVE**

